

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

SHULE YA SEKONDARI ITEWE  
S.L.P 169  
CHUNYA  
TAREHE 05/ 12/2020

PHONE:0767848017

KUMB: ITSS/ADM/01/VOL III/-

JINA LA MWANAFUNZI.....  
.....

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITEWE WILAYA YA CHUNYA MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.

### 1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifi kwamba umechaguliwa kijiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari ya Itewe mwaka 2021. Shule hii ipo umbali wa kilometra 1.5 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/ 01/ 2021**. Unatakiwa kuripoti shulenii tarehe **11/ 01/2021**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/ 01/ 2021** kwa watakaochelewa ndani ya siku saba baada ya kuanza masomo. Baada ya tarehe **18/01/2021** utakuwa umepoteza nafasi na atapewa mwanafunzi mwingine.

### 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:

#### 2.1 Sare za shule:

##### a. **Wavulana.**

Suruali mbili (2) moja rangi ya kijivu na ya pili rangi ya zambarau. Mashati mawili meupe mikono mifupi. **Maelezo ya mshono- wavulana suruali marinda mawili, isiyobana.**

##### b. **Wasichana**

Sketi mbili ndefu usawa wa (kifundo cha mguuni) moja rangi ya kijivu na ya pili rangi ya zambarau. Na mashati mawili meupe mikono mifupi.

#### **Maelekezo ya mshono – sketi marinda ya kawaida.**

**NB:-** Masweta mawili (2) moja ya rangi ya kijivu na la pili rangi ya zambarau shingo V, tai mbili moja rangi ya kijivu na nyingine rangi ya zambarau kwa wote Wavulana na Wasichana. Mzazi/Mlezi azingatie maelekezo ya mshono wa sare za shule. Tofauti na maelekezo **sare hiyo haitakubalika.**

- c. Sare ya michezo kwa shule hii ni **track suit nyekundu** yenye michirizi myeupe pamoja na raba kwa wasichana na wavulana.
- d. Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi kwa wote wavulana na wasichana, soksi nyeusi na mkanda mweusi kwa wavulana na soksi nyeupe kwa wasichana jozi mbili au zaidi.

**2.2 Vifaa vya usafi:** Njoo na mfagio mdogo na mkubwa (aina ya chelewa), ndoo mdogo moja, jembe ulaya lenye mpini moja kwa kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii.

**2.3 Vifaa vya kuandikia :** Njoo na daftari counter books kumi (10), kalamu za wino (biki), kalamu ya risasi ( penseli), rula, mkebe wenyenye vifaa vya Hisabati, jarada (file) la kumbukumbu binafsi.

**2.4 Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shulen ni kurudi nyumbani pamoja na matibabu** ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

**2 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama iliyovo rekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Toknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya RAIS- TAMISEMI yenyeye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kulipoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kutunza mali za umma na
- i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shulen:**

- (i) Wizi
- (ii) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
- (iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, au biashara ya madawa yote ya kulevyta.
- (iv) Makosa mengine ya jinai
- (v) Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzako au mtumishi
- (vi) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine

- (vii) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za Viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa.
- (viii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- (ix) Kuoa au kuolewa
- (xi) Kutoa au kushawishi kutoa mimba
- (xii) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
- (xiii) Kukataa adhabu halali.
- (xiv) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.
- (xv) Kujiachisha shule mwenyewe.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ni:

- a) Fomu ya kupima afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali baada ya kukupima afya yako. Form hii ikabidhiwe kwa Makamu wa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yaliyotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

#### KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....  
M.O.NJEJE

#### MKUU WA SHULE

**MKUU WA SHULE  
SHULE YASEKONDARI ITEMAI  
S .L .P . 169  
CHUNYA**

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

### SHULE YA SEKONDARI ITEWE

#### FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/ MLEZI

##### SEHEMU A: MWANAFUNZI:

- a) Mimi .....nilizaliwa  
tarehe.....Jina la Baba/Mlezi.....
- b) Jina la Mama/Mlezi .....nakubali  
kuingia kidato cha KWANZA katika shule ya Sekondari Itewe kama mwanafunzi,  
nitafika shulen tarehe ..... bila kukosa au kuchelewa.
- c) Nitattii sheria zote za shule kama zinavyonitaka na nitaishi maisha mazuri ya mfano  
hapa shulen. Nitakuwa mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.  
Sitakuwa mtoro shulen. Wala kuwa mwanafunzi mwenye usumbufu wa aina yoyote  
ile. Naahidi kutoshiriki migomo ya aina yoyote ile hapa shulen.
- d) Saini ya mwanafunzi.....tarehe.....

##### SEHEMU B: MZAZI

- 1. Mimi .....ninakubali mtoto wangu ( jina)  
.....asorhe katika shule ya Sekondari ya  
Itewe kuanzia tarehe .....naamini kuwa Elimu ni urithi wa  
mtoto na ni **UFUNGUO WA MAISHA**.
- 2. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shulen kama  
ulivyoagiza katika barua yako. Nitatoa na kutekeleza kwa wakati na bila  
usumbufu wowote.
- 3. Ninaahidi kuchangia mchango wa chakula cha mchana kama maelekezo ya  
serikali yanavyonitaka kufanya ili mwanangu apate chakula.
- 4. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na  
kuishi maisha mazuri na ya mfano kwa wenzake. Nitamhimiza asiwe mtoro na  
msumbufu.
- 5. Anuani yangu ya kudumu.....
- 6 Namba ya simu .....
- 7 Saini ya mzazi.....tarehe.....

##### SEHEMU C: KWA MATUMIZI YA OFISI TU.

- 1. Jina la mwalimu aliyempokea mwanafunzi.....
- 2. Ameleta/hajaleta mahitaji aliyoagizwa
- 3. Vitu alivyopungukiwa ni (taja).....
- 4. Saini ya mwalimu.....tarehe.....

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**SHULE YA SEKONDARI ITEWE S.L.P 169, CHUNYA**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili.....  
Dini/ dhehebu.....  
Tarehe ya kuzaliwa.....  
Shule ya msingi ulikosomea .....
2. Jina kamili la Baba mzazi / Mlezi.....  
Kazi yake.....  
Anwani yake .....,  
Namba ya simu ya mkononi.....  
Mahali anakoiishi baba  
mzazi/mlezi.Mkoa..... Wilaya..... Tarafa  
.....kijiji/Mtaa.....
3. Jina kamili la ma  
mzazi/mlezi.....  
Kazi yake.....  
Anwani yake.....  
Namba ya simu ya mkononi.....  
Mahali anapoisha mama mzazi/ mlezi : mkoa ..... Wilaya.....

**TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi .....

Nathibitisha kwamba taarifa nilizojaza hapo juu ni za kweli.

Sahihi ya mwanafunzi..... Tarehe.....

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

ITEWE SECONDARY SCHOOL  
P.O.BOX 169  
CHUNYA  
DATE.....

MEDICAL OFFICER  
GOVERNMENT HOSPITAL .....

P.O.BOX.....

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine..... ( student) as to her fitness for pursuing further Education at this school.

*[Signature]* .....  
HEADMASTER *HEADMASTER  
ITEWE SECONDARY SCHOOL  
BOX 169 CHUNYA*

Hemoglobin.....  
P.V Bleeding.....  
Blood Pressure.....  
Blood Group.....  
(a)Sight.....  
(b) Hearing.....  
6. Urine for sugar and pregnancy test.....  
7. Stool for routine – Examination.....  
8. Asthma .....,  
9. Skin diseases .....,  
10. Epilepsy .....,  
11. Leprosy .....,  
12. Pulmonary tuberculosis.....  
13. Deformity.....  
14. Mental problems.....  
15. V.D (Give Type).....  
16. Any other serious disease not mention above.....

OTHER COMMENTS.....  
.....  
.....  
.....

DESIGNATION AND SIGNATURE